MFUKO WA HIFADHI YA JAMII (ZSSF)



FIDIA SKIMU

UTANGULIZI

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar umeanzisha Skimu ya fidia chini ya sheria na.2 ya Mwaka 2005 kifungu na. 44 ambayo itasimamiwa na kuendesha shughuli zake chini ya

MAFAO YA KUUMIA KAZINI

Ni malipo yanayolipwa kwa mwanachama wa Mfuko pale anapopata maumivu yanayotokana na ajali, maradhi yatokanayo na kazi au kifo wakati au katika kutekeleza majukumu yake ya kazi.

AJALI NI NINI?

Ni tukio lililotokea bila kutarajia au kupanga katika kutekeleza majukumu ya kazi ya mfanyakazi husika ambalo limepelekea maumivu, ulemavu, maradhi au kifo cha mfanyakazi.

DHAMIRA YA SKIMU.

Fidia Skimu imedhamiria kupunguza athari za kijamii na kiuchumi za majanga yatokanayo na kazi kwa wafanyakazi kwa kutoa fidia stahiki kwa usawa endelevu na ufanisi.

KAZI NA MAJUKUMU YA SKIMU

a)Kupokea taarifa za ajali, maradhi yatokanayo na kazi na vifo na maombi ya fao la kuumia kazini.

b)Kuweka kumbukumbu na kutunza takwimu na taarifa za ajali, maradhi yatokanayo na kazi, vifo.

c)Kukusanya michango kutoka kwa waajiri.

d) Kulipa fao la kuumia kazini kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa katika Sheria na Kanuni za Skimu ya Fidia.

e) Kuimarisha mikakati ya kuzuia ajali, maradhi na vifo vitokanavyo na kazi.

f) kufanya maamuzi juu ya jambo lolote linalohusiana na haki ya mafao, hesabu za pato, kiwango cha ulemavu cha mfanyakazi na namna ya ulipaji wa fao la kuumia kazini na kuongeza kiwango cha fao la kuumia kazini;

g) Kutoa elimu na kujenga uwelewa kwa umma juu ya Skimu ya Fidia.

h) Kufanya kazi nyengine yoyote ambayo itakuwa muhimu katika kufanikisha malengo ya Skimu.

WAJIBU WA MWAJIRI

Kila mwajiri atakuwa na wajibu ufuatao katika Skimu:

a) Kulipa na kuwasilisha michango ya asilimia 1 (1%) katika Skimu katika utaratibu na muda ulioainishwa katika Sheria na Kanuni.

b) Kuwasilisha katika Skimu taarifa au ripoti ya ajali, maradhi yatokanayo na kazi au kifo cha mfanyakazi na taarifa zinazohusiana na ajali hiyo katika utaratibu na muda ulioainishwa katika kanuni.

c) Kutoa ushirikiano na kuisaidia Skimu katika namna inayowezekana kutekeleza majukumu yake ya kulipa fao la kuumia kazini.

WAJIBU WA MWANACHAMA

a) Kuliomba fao pale atakaporipoti kazini baada ya kumaliza matibabu ya msingi.

b) Kutoa taarifa za ukweli .

c) Kutoa ushirikiano kwa Daktari pale atakapotathminiwa wakati wa kujaziwa fomu ya tathmini.

MICHANGO

Skimu inajengeka kutokana na michango ya wanachama. Mshahara wa mwanachama ndio kigezo cha kuchangia. Sheria inamtaka mwajiri awasilishe asilimia moja (1%) ya mshahara wa mwanachama bila ya kukata mshahara wa mwanachama kwa kila mwezi kipindi mwanachama huyo yupo kwenye ajira. Ili mwanachama astahili kulipwa fao la kuumia kazini ni lazima awe amechangia angalau mwezi mmoja.

VYANZO VYA FEDHA ZA SKIMU

Vyanzo vya Fedha vya Skimu vitakuwa:
a) Michango itakayolipwa na waajiri kama ilivyoanishwa katika sheria;

b) Fedha zitakazolipwa na waajiri chini ya masharti ya sheria;

c) Adhabu zitakazotozwa chini ya masharti ya sheria;

d)Mapato yatokanayo na uwekezaji wa fedha za Skimu; na

e)Fedha yoyote itakayopatikana kihalali na Skimu.

ANAESTAHIKI KULIPWA FAO LA KUUMIA KAZINI

Mwanachama yeyote ambaye ameajiriwa na kusajiliwa na Mfuko wa hifadhi ya Jamii, Zanzibar na ambaye amechangia angalau mwezi mmoja wa ajira na anaendelea na kazi wakati tukio la ajali linapotokezea.

Mwanachama yoyote ambaye amepata ajali akiwa katika mazingira ya kazi.
Mtu yeyote ambaye anamuuguza mwanachama aliyepata maumivu ya kudumu.

AINA ZA MAFAO

a)Fao la maumivu ya muda;

b)Fao la ulemavu wa kudumu ambao haukumzuia kurudi kazini;

c)Fao la ulemavu wa kudumu ambao umemzuia kurudi kazini tena;

d)Fao kwa anaemuhudumia mgonjwa asiejiweza ukiondoa muuguzi/ muhudumu wa afya alieajiriwa kufanya kazi hiyo.

e)Fao la kifo;

1. Fao la maumivu ya Muda



Fao la Maumivu ya muda litalipwa kwa mfanyakazi atakaepata maumivu kutokana na ajali au maradhi yatokanayo na kazi wakati au katika kutekeleza majukumu yake ya kazi ambayo yamesababisha ulemavu wa muda kwa mfanyakazi huyo.

Fao la kupatwa na majeraha na ulemavu wa muda litakokotolewa kulingana na majeraha

na maradhi kwa kuzingatia idadi ya siku ambazo mfanyakazi hakuweza kuhudhuria kazini kwa ruhusa ya daktari.

Fao la Maumivu ya muda litakuwa nusu ya pato la siku la mfanyakazi likizidishwa na idadi ya siku ambazo mfanyakazi hakuhudhuria kazini kutokana na maumivu aliyoyapata kwa ajali.

2.Fao la Ulemavu wa Kudumu



Fao la Maumivu ya kudumu litalipwa kwa mfanyakazi atakaepata ajali au maradhi yatokanayo na kazi wakati au katika kutekeleza majukumu yake ya kazi ambayo yamesababisha ulemavu wa kudumu kwa mfanyakazi huyo.

Fao la Ulemavu wa kudumu litakokotolewa kwa kigezo cha asilimia ya ulemavu husika ya kima cha mshahara wa miezi 48. Fao hili litaambatana na Fao la maumivu ya muda.

3. Fao la Kifo



Fao la Kifo litalipwa kwa wategemezi wa mfanyakazi aliefariki akiwa anatekeleza majukumu yake ya kazi au amefariki kutokana na maradhi yanayotokana na kazi au ajali iliyompata wakati akitekeleza majukumu yake ya kazi iliyosababisha kifo cha mfanyakazi husika.

Fao la kifo litalipwa kwa wategemezi wa mfanyakazi aliefariki mara moja tu kwa mkupuo ambalo litakuwa sawa na mishahara ya miezi 48 ya mfanyakazi husika.

Fao la kifo litakalolipwa ni sehemu ya mali ya mfanyakazi husika na litalipwa kwa wategemezi wa mfanyakazi aliefariki kupitia Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar kwa mfanyakazi Muislamu na Mkurugenzi Wakala wa Usajili wa Mali na Biashara Zanzibar kwa mfanyakazi asiyekuwa Muislamu.

4. Fao kwa mtu anaemuhudumia Mgonjwa.

Fao hili litalipwa kwa mtu wa karibu au mtu mwengine yeyote anaemuhudumia mfanyakazi aliepata ulemavu wa kudumu na asiejiweza kujifanyia huduma zake muhimu za kimaisha bila ya kuwa na mhudumu kutokana na ajali au maradhi yatokanayo na kazi.

Kiwango cha Fao la mtu anaemuhudumia mfanyakazi aliepata ulemavu wa kudumu asiejiweza kujihudumia mahitaji yake muhimu ya kimaisha kutokana na ulemavu litakuwa robo ya kiwango cha fao la ulemavu wa kudumu alicholipwa mfanyakazi husika na litalipwa kwa mkupuo mara moja tu.

VIGEZO VYA KUOMBA MAFAO.

Katika maombi ya fao la kuumia kazini mambo yafuatayo yatazingatiwa:-

1) Iwapo ajali au maradhi yatokanayo na kazi au kifo kimetokea katika utekelezaji wa majukumu ya kazi ya mfanyakazi.

2)Iwapo mfanyakazi amepata maumivu au kafariki kutokana na ajali au maradhi yatokanayo na kazi.

3)Iwapo mfanyakazi amepata ulemavu kutokana na ajali au maradhi yatokanayo na kazi.

4)Iwapo ajali imetokana na utekelezaji wa majukumu ya kazi ya mfanyakazi.

5)Iwapo mwajiri wa mfanyakazi husika amewasilisha michango inayotakiwa katika

Skimu.

6) Iwapo mfanyakazi aliye nje ya Zanzibar aliruhusiwa au kuidhinishwa na mwajiri kutekeleza au kuhudhuria kazi hiyo;

7) Kutolewa kwa ripoti ya daktari na ushahidi ambao unaweza kuhitajika kuhusiana na maombi hayo ya mafao.
Fao la Kuumia Kazini halitalipwa kutokana na maumivu au ulemavu wa muda wa chini ya siku 3.

MAOMBI YA MAFAO.
Maombi ya fao la kuumia kazini yatafanywa na mfanyakazi au mtu mwengine kwa niaba ya mfanyakazi kwa Mkurugenzi Mwendeshaji mara tu mfanyakazi ataporipoti kazi baada ya kupoa majeraha, au ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kugundulika maradhi yatokanayo na kazi, na ndani ya siku thelathini (30) kwa mwanachama aliyefariki. Maombi hayo yataombwa kwa kujaza fomu ya maombi ya Mafao hayo (SSF 18) yakiambatanishwa na:

a) Nakala ya kadi ya uanachama ya ZSSF.

b) Cheti cha kifo (Kwa mwanachama aliefariki)

c) Taarifa ya daktari.

d) Hati ya Polisi (PF3 au PF90).

e) Slipu ya mshahara.

f) Karatasi ya kuhudhuria Hospitali.

g) Taarifa ya ruhusa ya kutoka Hospitali.

h) Taarifa nyengine yoyote ambayo itakuwainafaa.

i) Taarifa ya Bodi ya Madaktari (Kwa mwanachama aliepata ulemavu uliomfanya asiweze tena kurejea kazini)
Maombi ya fao la kuumia kazini hayatazingatiwa endapo hayatawasilishwa kwa Mkurugenzi Mwendeshaji.

MUDA WA KULIPA MAFAO.
Maombi yote ya fao la kuumia kazini yatalipwa ndani ya muda wa wiki mbili (2) hadi nne (4) baada ya kuwasilisha fomu ya tathmini ya Maumivu iliyojazwa na Daktari.

MFUMO WA KULIPA MAFAO.
Malipo ya fao la kuumia kazini yatafanywa kwa njia ya mkupuo mara moja tu kwa njia ya benki au kama itakavyoelekezwa na Mkurugenzi Mwendeshaji.

ADHABU.
Mwajiri, Mwanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Zanzibar au mtu yeyote atakayelipwa Fao la Fidia kupitia Fidia Skimu atastahiki kuadhibiwa Kisheria na iwapo atatiwa hatiani ikiwa atafanya makosa yafuatayo atatozwa faini ya shilingi za Kitanzania Milioni tano (5) au Kifungo kisichopungua mwaka mmoja (1) Chuo cha mafunzo au adhabu zote mbili kwa pamoja:-

a) Iwapo atashindwa kulipa au kuwasilisha michango au adhabu katika Skimu kwa wakati ulioelezwa.

b) Iwapo atashindwa kutoa nyaraka au taarifa zinazotakiwa.

c) Iwapo atakapopunguza au atasita kukata kutoka kwa mfanyakazi kiasi chochote kuhusiana na michango katika Skimu.

d) Iwapo atakwepa kulipa michango yeye mwenyewe au mtu mwengine yeyote.

e) Iwapo atatoa taarifa ambazo sio sahihi au za uongo.

f) Iwapo atawasilisha au kusababisha kuwaslishwa nyaraka au taarifa ambazo anajua kwamba ni za uongo.

g) Iwapo atashindwa kutii na kufuata ipasavyo taratibu za ulipaji wa Fao la kuumia kazini.

h) Iwapo atajipatia isivyo halali fao la kuumia kazini yeye mwenyewe au kwa mtu mwengine.

i) Iwapo atazuia au kumshambulia mfanyakazi yeyote wa Skimu katika kutekeleza majukumu yake.